



USAID

KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI

SERA YA KUIMARISHA UWEZO WA WAZAWA

Muhtasari

Sera ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa (Local Capacity Strengthening - LCS) inaongoza maamuzi ya USAID kuhusu kwa nini na jinsi ya kuwekeza katika uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali kulingana na kanuni zinazotokana na makubaliano ya kujitokeza katika mazingira ya maendeleo, mrejesho kutoka kwa wadau wa sekta mbalimbali na washirika, na uzoefu wa miaka ya utekelezaji na ushahidi.



Sera ya LCS **inathibitisha kujitolea kwa USAID kwa kuimarisha uwezo wa wazawa** kwa kuweka wazi **kanuni saba** zinazoongoza msaada wa kibinadamu wa USAID na programu ya maendeleo.

Wakati mbinu za kuimarisha uwezo zinatofautiana kulingana na sekta na muktadha, Sera ya LCS inaipa Taasisi mfumo shirikishi ili kuleta programu ambayo **inajenga zaidi uwezo uliopo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali na mifumo ya ndani, inajibu vipaumbele vya wazawa vinavyobadilika, na inalingana na malengo ya kimkakati ya USAID.**

Kwa pamoja, kanuni na mwongozo ulioainishwa katika Sera ya LCS utasaidia USAID **kusaidia wadau kutoka katika sekta mbalimbali kufikia malengo yao, kuongoza maendeleo ya jamii zao, na kuunda mustakabali wa nchi zao.**



KUENDELEZA MAENDELEO YANAYOSIMAMIWA NA WAZAWA

Maendeleo ya sasa ya kidunia na changamoto za kibinadamu ni kubwa, zinahitaji kufanyiwa kitu, na ni ngumu kushughulika nazo. Changamoto hizi zinarithiwa miongoni mwa wazawa, zinaundwa na historia ya kipekee, uhusiano wa kiutawala miongoni mwa sekta mbalimbali, na mambo mengine maalum kwa kila muktadha ambao hutokea. Maendeleo yanayosimamiwa na wazawa ni mchakato ambao wadau kutoka katika sekta mbalimbali huweka ajenda zao wenyewe, kuendeleza ufumbuzi, na kuleta uwezo, uongozi, na rasilimali za kufanya ufumbuzi huo kuwa unaowezekana.

USAID inatambua kwamba uongozi na umiliki wa wazawa ni muhimu kwa kukuza matokeo endelevu katika kazi zetu za kimaendeleo na misaada yetu ya kibinadamu. Kuthamini na kujenga uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali ni sehemu ya msingi ya programu ya USAID, na Sera ya LCS inaashiria hatua muhimu katika kufikia malengo ya Taasisi ya ujanibishaji.

Picha imepigwa na:
(Picha ya juu) USAID/Philippines;
(Picha ya kati) Feed the Children/Amos Gumulira

KANUNI SABA ZA KUIMARISHA UWEZO WA UFANISI NA USAWA

Sera imepangwa kwa **kanuni saba za kuimarisha** pande zote ili kusababisha **programu bora zaidi na ushirikiano wa usawa** katika shughuli za kuimarisha uwezo wa wazawa.

- **Kanuni za ufanisi wa programu** zinaongoza ufahamu wetu kuhusu kwa nini na katika hali gani kufanya maamuzi ya kimkakati na ya makusudi ili kuimarisha uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali kama sehemu ya Mzunguko wa Programu ya USAID inaweza kuchangia mabadiliko mapana ya mifumo na matokeo endelevu. Kanuni hizi pia zinaongoza uelewa wetu kuhusu kwa nini kupima utendaji ni muhimu.
- **Kanuni za ushirikiano wa usawa** huweka maadili ya kuheshimiana na usawa ili kuongoza programu ya Taasisi ya kuimarisha uwezo kwa wazawa katika sekta na kanda mbalimbali.

Ofisi zitaendeleza mwongozo maalum wa kissekta kulingana na kanuni hizi ili kuleta programu zao.



Picha imepigwa na: Bobby Neptune kwa ajili ya USAID

KUANZIA KANUNI HADI UFANYAJI KAZI

USAID itatekeleza Sera ya LCS kupitia maeneo manne ya kipaumbele yanayoingiliana:

1. Tengeneza mwongozo muhimu wa utekelezaji pamoja na nyenzo, ukihusisha muktadha wa kissekta.
2. Unda njia za uwajibikaji na maoni ili kuendeleza utekelezaji wa Sera ya LCS.
3. Saidia ushirikiano wa LCS katika programu na kuza uwezo wa USAID kutekeleza Sera.
4. Tuma ushahidi na hadithi ili kuonesha umuhimu wa kuimarisha uwezo wa wazawa na kuhimiza zaidi kutekeleza Sera.

KANUNI KWA AJILI YA PROGRAMU YENYE UFANISI

- 1 Anza na mfumo wa wazawa.
- 2 Iimarisha uwezo tofauti kupitia njia mbalimbali.
- 3 Panga na pima uboreshaji wa utendaji kwa kushirikiana na washirika wazawa.

KANUNI ZA USHIRIKIANO WENYE USAWA

- 4 Pangilia uimarishaji wa uwezo na vipaumbele vya wazawa.
- 5 Thamini na jenga uwezo uliopo.
- 6 Kumbuka na punguza matokeo yasiyotarajiwa ya msaada wetu kwa uimarishaji wa uwezo wa wazawa.
- 7 Fanya kazi kwa kufuata ushirikiano wa kiutendaji baina ya washirika wazawa.

Tembelea [ukurasa wa Sera ya LCS](#) ujifunze zaidi kuhusu Sera ya USAID ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa, tafuta nyenzo za utekelezaji wa sera, na ugundue fursa za kushiriki.